

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU



OFISI YA MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
S.L.P 74, MBULU

23/09/2019

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MUDA

Kwa mujibu wa Kifungu cha 10 (2) cha Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti Wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji za Mwaka 2019

Msimamizi wa Uchaguzi Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu anapenda kuwajulisha kuwa, zoezi la kujiandikisha katika Orodha ya Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Vijiji 76 na Vitongoji 361 vya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu litaanza tarehe 8/10/2019 hadi 14/10/2019.

Hivyo Msimamizi wa Uchaguzi anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania kwa nafasi ifuatayo:

MWANDIKISHAJI ORODHA YA WAPIGA KURA

A. Sifa za mwombaji wa nafasi ya Mwandikishaji Orodha ya Wapiga Kura

1. Awe raia wa Tanzania.
2. Awe Mtumishi katika Utumishi wa Umma (Public Service)
3. Awe anafanya kazi katika Kata / Kijiji husika anachoombea.
4. Awe na elimu ya kuanzia Kidato cha nne na ajue kusoma na kuandika.
5. Asiwe na dhamana au Uongozi au kada wa Chama cha Siasa.
6. Awe mwadilifu na mwaminifu.
7. Asiwe Mtendaji wa Kijiji na Kata

B. Majukumu ya Mwandikishaji Orodha ya Wapiga Kura

1. Kuhakikisha kuwa kituo kinafunguliwa kwa wakati na kuanza uandikishaji kwa muda uliopangwa ambao kwa mujibu wa maelekezo ni saa 2:00 Asubuhi hadi saa 12:00 jioni.
2. Kubandika bango la Kituo cha Kuandikisha Wapiga Kura na mabango mengine yaliyotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kituo cha uandikishaji.
3. Kuhakikisha vifaa muhimu vya kituo vinakuwepo katika Kituo cha kuandikisha Wapiga Kura.
4. Kuwepo kituoni muda wote wa kazi hata kama hakuna Wapiga Kura wanaokuja kujandikisha.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU

5. Kuhakikisha kuwa Wanaojiandikisha kuwa Wapiga Kura waliokuja kituoni kabla ya saa 12:00 jioni na kupanga foleni wanaandikishwa wote isipokuwa kama wapo wengi, wataorodheshwa majina na kuwapanga kuanza nao siku inayofuata.
6. Kuhakikisha kuwa baada ya uandikishaji wa siku kukamilika, taarifa ya Wapiga Kura walioandikishwa kwa siku hiyo inaandaliwa na kutunzwa kwa lengo la kumkabidhi Msimamizi Msaidizi ngazi ya Kata.
7. Kuhakikisha kuwa vifaa na nyaraka za uandikishaji vinatunzwa vizuri kipindi chote cha zoezi na kuvikabidhi kwa Msimamizi wa Uchaguzi vikiwa katika ubora wake baada ya zoezi kukamilika.
8. Majukumu mengine atakayopangiwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

C. Mambo ya kuzingatia wakati wa kutuma maombi

1. Mwombaji lazima aainishe kazi anayoomba ambayo ni: **Mwandikishaji Orodha ya Wapiga Kura**
2. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika na picha 3 (Passport Size) za hivi karibuni.
3. Maombi yote yatapaswa kuambatana na nakala za vyeti vya kitaaluma na kitaalamu.
4. Mwombaji (Mtumishi wa Umma) atapaswa kupidisha maombi kwa **Mtendaji wa Kata** husika.
5. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 30/09/2019
6. Maombi yote yatumwe kupidisha anuani ifuatayo;


**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA WILAYA**

**SLP 74
MBULU**

Email: md@mbuludc.go.tz

**NB: TANGAZO HILI UNAWEZA KULIPATA KUPITIA TOVUTI YETU:
www.mbuludc.go.tz**

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA



**HORACE KOLIMBA
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA WILAYA**

MBULU

**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA WILAYA
MBULU**